**Serikali >>> Imetoa kipaumbele katika matumizi ya TEHAMA, hususan masuala ya utafiti na ubunifu pamoja na kuimarisha usalama wa mtandao wa mawasiliano**

# Dk. Manguruwe azidi kusota rumande

**Dar es Salaam**
**NA REHEMA MOHAMED**

UPELELEZI wa kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Mkurugenzi mwanzilishi wa Kampuni ya Vanilla International Limited, Simon Mkondya maarufu kama Dk. Manguruwe na mwenzake, haujakamilika.

Wakili wa Serikali, Erick Device alidai hayo juzi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam wakati kesi hiyo ilipotajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Anna Magutu.

Kutokana na hali hiyo, wakili huyo aliiomba mahakama ipange tarehe nyingine ya kutajwa ambapo ilipangwa Februri 26 mwaka huu. Mshitakiwa mwingine katika kesi hiyo ni Rweymamu John ambaye ni mkaguzi wa kampuni hiyo.

Washitakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na jumla ya mashitaka 28 yakiwemo ya kujipatia zaidi ya sh. milioni 90 kwa udanganyifu na utakatishaji kwa kununua viwanja tisa eneo la Idunda Mkoa wa Njombe.

Ilidaiwa kwamba washitakiwa hao walitenda makosa hayo katika tarehe tofauti kati ya Januari mosi mwaka 2020 na Desemba mosi mwaka 2023 ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam

Ilidaiwa kwamba mashitaka 19 ni ya kufanya biashara ya upatu, ambapo katika kipindi hicho Mkondya akiwa kama mkurugenzi na John akiwa kama mfanyakazi wa kampuni hiyo walifanyabiashara ya upatu kwa kuwaahidi watu kupata faida mara mbili hadi tatu kulingana ya kiasi cha fedha watakazotoa.

Aidha, ilidaiwa kwamba washitakiwa hao walijipatia kiasi cha jumla ya sh. milioni 92.2 kutoka kwa watu 19 tofauti ambapo watu hao walitoa kiasi tofauti cha fedha akiwaahidi watapata faida mara mbili hadi tatu ya fedha walizotoa.

Iliendelea kudaiwa kwamba, mashitaka tisa ni ya utakatishaji yanayomkabili mshitakiwa Mkondya pekee ambapo katika kipindi kati ya Januari mosi mwaka 2020 na Desemba mosi 2023 akiwa kama Mkurugenzi wa kampuni hiyo, alijipatia jumla ya viwanja tisa kitalu namba AB eneo la Idunda mkoani Njombe huku akijua viwanja hivyo ni mazalia ya makosa tangulizi ya upatu.

# Simbachawene atoa maagizo matumizi ya mtandao

**Arusha**
**NA MWANDISHI WETU**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amezitaka taasisi za umma ambazo bado zina kiwango kidogo cha utekelezaji jitihada za serikali mtandao kuongeza kasi ya matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuleta tija katika utendaji kazi.

Simbachawene alisema hayo jana alipokuwa akifunga kikao kazi cha tano cha Serikali Mtandao kilichofanyika katika ukumbi wa AICC jijini hapa ambacho kilihudhuriwa na wadau takriban 1500.

Alisema serikali imedhamiria kuimarisha na kuongeza matumizi TEHAMA kwenda sanjari na maendeleo ya sayansi na teknolojia kwa kuwa shughuli nyingi duniani zikiwemo za kiuchumi hivi sasa zinafanyika kwa kutumia TEHAMA.

Waziri huyo alibainisha kuwa serikali imetoa kipaumbele katika matumizi ya TEHAMA, hususan masuala ya utafiti na ubunifu, kuimarisha usalama wa mtandao wa mawasiliano na kuongeza watumiaji wa intaneti.

Alieleza kuwa wizara kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) imejipanga kupanua wigo upatikanaji huduma mtandao kwa umma kidijitali na kuboresha upatikanaji mawasiliano ya simu nchi nzima ili kuwawezesha Watanzania kupata huduma kwa wakati na kwa gharama nafuu.

"Tunajivunia kuona idadi ya watumiaji wa simu za mkononi na intaneti, inaongezeka mwaka hadi mwaka. Ongezeko hili linatupa chachu kuboresha upatikanaji huduma za serikali kupitia simu za mkononi na linadhihirisha ongezeko la matumizi ya TEHAMA hapa nchini," alisisitiza.

Waziri Simbachawene alizitaka taasisi za umma kuchukua hatua za haraka kuhakikisha zinatumia fursa ya ongezeko hilo kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi kidijitali kupitia simu za mkononi.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Ikulu, Mulula Mahendeka, alisema vikao vinavyofanyika vinaa manufaa katika kukuza na kuendeleza jitihada za Serikali Mtandao, kupitia mawazo mbalimbali yanayotolewa na washiriki wa vikao.

Mahandeka alisema wizara itasimamia utekelezaji wa maazimio yote yaliyofikiwa katika kikao hicho kwa wakati, e-GA au taasisi nyingine ya umma inayohusika.

Naye, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Mhandisi Benedict Ndomba, aliwashukuru washiriki kwa umakini, utulivu na usikivu walioonesha wakati wote wa kikao hali iliyochangia kupata mawazo bora wakati wa majadiliano.

Alisema mawazo yaliyotolewa ni chachu katika maendeleo ya Serikali Mtandao na mamlaka itayafanyia kazi maoni na mapendekezo yote yaliyotolewa kwa kuwa na jitihada za Serikali Mtandao zenye tija zaidi.

# Kamati CDC zapewa somo matumizi fedha za CSR

**Musoma**
**NA MWANDISHI WETU**

MGODI wa Barrick North Mara uliopo mkoani mara umewezesha wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii (CDC) mkoani Mara kupata mafunzo ya uibuaji miradi ya kijamii yenye tija inayotekelezwa na fedha za uwajibikaji kwa jamii inayotolewa na mgodi huo.

Katika hotuba ya ufunguzi wa mafunzo hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi, alionyesha kutoridhishwa na maendeleo ya wananchi wa vijiji vinavyopokea fedha za uwajibikaji kwa jamii (CSR) na mirabaha kutoka Mgodi wa Barrick Dhahabu wa North Mara.

Alisema vijiji hivyo vya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime (Vijijini) vinapokea fedha kila mwaka za maendeleo, lakini maisha ya wananchi wake hayajaboreka kutokana na viongozi kutowajibika kikamilifu katika kuzisimamia zitumike kwa ufanisi.

"Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ni miongoni mwa halmashauri zenye utajiri mkubwa hapa nchini, mgodi unafanya kazi kubwa kuchangia miradi ya maendeleo kwa kutoa CSR na mrabaha, lakini bado fedha hizo hazijaleta matarajio mazuri kwa wananchi," alisema.

Matambi alisema viongozi wa vijiji hivyo kuhakikisha wanaibua miradi ambayo ni kipaumbele cha wananchi na kutumia vizuri fedha hizo ili kuleta mabadiliko chanya.

Alisema hatasita kuingilia kati na kubadilisha matumizi ya fedha hizo iwapo miradi itakayoibuliwa na viongozi haitakidhi matakwa ya wananchi wa vijiji hivyo.

Pia, Matambi aliushukuru mgodi wa Barrick North Mara kwa kuandaa mafunzo hayo kwa viongozi hao pamoja na mchango wake mkubwa kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime na Mkoa wa Mara kwa ujumla.

Matambi aliwahimiza washiriki wa mafunzo hayo kwenda kuyafanyia kazi kwa vitendo katika maeneo yao, ikiwemo kuimarisha utendaji wao wa kazi na kutatua kero za wananchi.

Mtambi alitoa wito kwa wakazi wa eneo la Nyabirama 171 ambao bado hawajachukua fidia zao kujitokeza kuzichukua na wale 11 waliogomea fidia kupisha uwekezaji wa mgodi wa North Mara waendelee kuelimishwa kuhusu umiliki wa ardhi na athari za wao kuendelea kuishi hapo wakati shughuli za mgodi zikiendelea.

Kwa upande wake, Meneja Mkuu wa Mgodi wa Barrick North Mara, Apolinary Lyambiko, alisema wajumbe wa CDC wanaoshiriki mafunzo hayo wamo viongozi wapya waliopatikana katika uchaguzi wa serikali za mitaa uliopita na lengo lake ni kuwajengea uelewa kuhusu utawala bora, usimamizi wa sheria na uwajibikaji katika majukumu yao.

Naye Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini, Mwita Waitara alisema fedha za CSR na mrabaha zinazotolewa zikitumika vizuri zitaifanya halmashauri ya wilaya hiyo kuwa mfano bora kwa maendeleo ya jamii.

Kwa upande wa mshiriki wa mafunzo hayo, Diwani wa Kata ya Nyarokoba, Juma Matiko, alisema mafunzo hayo yatawafanya wawajibike kwa waledi ikiwemo kusimamia vizuri matumizi ya fedha zinazotolewa na mgodi kwa maeneo yao.


## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

**TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA PWANI NA TANGA KATIKA HALMASHAURI ZA WILAYA ZA LUSHOTO, KILINDI, MUHEZA, KOROGWE, MJI WA KOROGWE, MJI WA HANDE NA JIJI LA TANGA.**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza unafanyika katika Mikoa ya Pwani na Tanga katika Halmashauri za Wilaya za Lushoto, Kilindi, Muheza, Korogwe, Miji ya Korogwe na Handeni na Jiji la Tanga tarehe 13 hadi 19 Februari, 2025. Zoezi la uboreshaji wa Daftari linafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. **SIKU:** Uboreshaji unafanyika kuanzia siku ya Alhamisi tarehe 13 hadi siku Jumatano tarehe 19 Februari, 2025,
2. **VITUO:** Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyomo katika Mitaa, vijiji na vitongoji,
3. **MUDA:** Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji utahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa miaka 18 na zaidi ambao hawakuwahi kuandikishwa hapo awali, na ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
2. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi (Jimbo au Kata).
3. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
4. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
5. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili kwa pamoja, wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume ***www.inec.go.tz*** au anuani ya ***ovrs.inec.go.tz*** kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la Kata anayokusudia kuhamia, kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo katika kituo cha kuandikisha Wapiga Kura ili kukamilisha taratibu na kupatiwa kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo (maarufu kama kitochi au kiswaswadu) anaweza kuingia kwenye mfumo wa OVRS kwa kupiga *152*00#, kisha, atachagua namba 8 na kubonyeza, kisha atachagua namba 2, kisha atabonyeza namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga simu namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali na hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

Limetolewa tarehe 04 Februari, 2025 na:

Saida H. Mohammed
**KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI**